**NAFASI YA MAKTABA ZA UMMA NCHINI**

*Na: Gibson, J.E Mdakama; Agosti 2018*

## UTANGULIZI

Maktaba za umma ni moja ya vyombo muhimu sana katika ukuaji wa ubora wa elimu nchini. Umuhimu wa kuwa na maktaba za umma nchini kwa sasa umekuwa ni sehemu kuu ya mahitaji ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla katika kuhakikisha taifa linasonga mbele katika Maendeleo ya Elimu pamoja na uchumi wa nchi hasa kuifikia nchi ya uchumi wa viwanda kama tulivyojiwekea malengo hayo kupitia Sera ya Maendeleo ya nchi ya 2014/15-2024/25.

Kutokana na umuhimu huo mkubwa ambao unatokana na mchango wa uwepo wa maktaba katika kizazi chetu cha sasa, kizazi ambacho jamii yake imepiga hatua, jamii ambayo tumeazimia kuifikisha nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2024/25, hilo ndilo kusudi na sababu iliyopelekea kutushawishi hasa kufanya utafiti juu ya umuhimu wa uwepo wa maktaba na mchango wake katika kukuza maendeleo ya elimu pamoja na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Makala haya yameandikwa kutokana na utafiti huo, ambao ulifanyika katika mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya Moshi Vijijini mwaka 2018. Utafiti huu umefanywa na Ndugu GIBSON J.E Mdakama (Mratibu wa Mtandao Wa Wanafunzi Tanzania-TSNP Mkoa wa Kilimanjaro na ambae pia ndie mwandishi wa makala haya) kwa kushirikiana na Idara ya Tafiti na Mafunzo Mtandao wa Wanafunzi Tanzania (TSNP).

Utafiti huu ulifanyika katika shule 50; kati ya hizo, shule 20 ni za sekondari na 30 ni za msingi zilizoko katika kata 10 za wilaya ya Moshi Vijijini. Aidha, katika utafiti huu, taarifa mbalimbali zilitokana na mapitio ya maandiko mbalimbali pamoja na maoni ya walengwa ambao tuliwafikia. Walengwa hao ni: Maofisa wa elimu kata 3, walimu wakuu 50, walimu 35(15 ni wa shule ya msingi na 20 ni wa Sekondari)na Wanafunzi 140(60 ni wa Shule ya Msingi na 80 ni wa Sekondari).

Makala hii imekusudiwa iwe chachu kwa jamii na taifa kwa ujumla kufumbua macho na kutoka usingizini kuhakikisha kuwa tunatia mkazo katika kuhakikisha kuwa angalau kwa kila wilaya ama jimbo ama kata kunakuwa na maktaba bora ili kuwawezesha wanafunzi na jamii kwa ujumla kuchota maarifa.

*Makala hii inajumuisha mambo yafuatayo:*

i. Hali halisi ya uwepo wa maktaba nchini katika shule za umma za Msingi na Sekondari.
ii. Matokeo ya kipengele cha kwanza hapo juu katika kuleta tija kwenye maendeleo ya Elimu na uchumi wa nchi yetu.
iii. Umuhimu, nafasi na mchango wa maktaba za umma katika kukuza na kudumisha maendeleo ya Elimu na nchi kwa ujumla.
iv. Rasilimali zilizopo nchini na umuhimu wake katika kuanzisha, kudumisha na kuendeleza ama kuzistawisha maktaba za umma nchini.
v. Makala hii itahitimisha kwa kuyaainisha mapendekezo ya wadau mbalimbali katika kuendeleza na kuboresha hali ya maktaba za umma nchini katika mgawanyo sawia wa uhusiano wake na rasilimali zilizopo kama tutakavyozibainisha kwenye kipengele namba (iv) hapo juu.

## *1.0: HALI HALISI YA UWEPO WA MAKTABA KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI ZA UMMA NCHINI.*

Nafasi na umuhimu wa maktaba katika shule zetu za umma unachukua sura pana sana katika maendeleo ya shule hizi kitaaluma. Hii ni kutokana na kwamba maktaba humwezesha mwanafunzi kupata maarifa zaidi katika kile anachojifunza na anachotaka kujifunza ndani na nje ya darasa.

Hali iliyo tofauti ni kwamba, hili limekuwa kinyume kabisa katika shule zetu za Msingi na sekondari nchini, shule nyingi hazina maktaba bora na zenye vitabu vya kutosha kuwezesha wanafunzi kuyachota maarifa yatakayowasaidia katika kuimarisha taaluma zao. Hali hii imekuwa ikizidi kutamalaki na kuota mizizi kutokana na viongozi wa serikali wakionyesha kufumbia kabisa macho suala la

upatikanaji wa maktaba nchini ama kutoona umuhimu wa uwepo wa maktaba nchini ama kupuuzia na hivyo kutoona haja yoyote ya kutoa tathmini juu ya uwepo wa maktaba nchini.

Katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2017/218, jedwali Na. 8-7 linaloonyesha muhtasari wa miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari, hajataja kabisa mchanganuo wa uwepo wa maktaba nchini. Tazama kielelezo kifuatacho.




**Jedwali Na. 8-7:Muhtasari wa hali ya miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari**

| Maelezo | Mahitaji | Iliyopo | Upungufu | % |
|---|---|---|---|---|
| **Shule za Sekondari** | | | | |
| Vyumba vya Madarasa | 24797 | 12001 | 12796 | 52 |
| Maabara | 6772 | 1065 | 5707 | 84 |
| Matundu ya Vyoo | 33652 | 15913 | 17739 | 53 |
| Madawati | 211197 | 28637 | 182560 | 86 |
| Nyumba za walimu | 6879 | 1041 | 5838 | 85 |
| Mabweni | 11461 | 1366 | 10095 | 88 |
| | | | | |
| **Primary school** | | | | |
| Vyumba vya Madarasa | 83369 | 12790 | 70579 | 85 |
| Matundu ya Vyoo | 105776 | 18272 | 87504 | 83 |
| Madawati | 246303 | 212255 | 34048 | 14 |
| Nyumba za walimu | 14257 | 4868 | 9389 | 66 |

Aidha, katika chapisho lililotolewa na tovuti ya www.nukta.co.tz la tarehe 06 Juni, 2018 lilieleza kuwa; halmashauri ya wilaya ya Kyela mkoani Mbeya ina uhitaji wa maktaba 102 ili kuwasaidia wanafunzi wa shule za msingi wilayani humo kupata fursa ya kujiongezea maarifa kwa kujisomea vitabu lakini mpaka sasa hakuna hata maktaba moja.

Kwa upande wa Zanzibar, kwa mujibu wa Shirika la Huduma za Maktaba, takribani asilimia 60% ya shule za msingi hazina maktaba na asilimia 30% ya shule za Sekondari hazina maktaba pia.

Hata hivyo, Takwimu za Elimu ya Msingi Tanzania (BEST) za mwaka 2016 zinazitaja wilaya nyingi nchini kutokuwa na maktaba za kutosha. Hapa chini ni kielelezo kinachoonesha hali ilivyo kwa Mkoa wa Mbeya kama ilivyoainishwa na BEST.




Hivyo basi, tunaamini kwa utafiti huu tulioufanya kwa wilaya ya Moshi Vijijini utakuwa kama rejea ya uwepo wa maktaba katika Wilaya na Mikoa mingine nchini.

### *1.1: MCHANGANUO WA HALI HALISI YA UWEPO WA MAKTABA KATIKA WILAYA YA MOSHI VIJIJINI MKOA WA KILIMANJARO.*

Katika shule za msingi za umma tulizozipitia tumegundua kuwa, miongoni mwa shule zote 30, hakuna hata shule moja yenye maktaba ambayo inavifaa vyote vinavyohitajika katika maktaba.

Aidha, kati ya shule hizo, ni shule 13 tu zenye vitabu vya kutosha vya masomo yote, masomo hayo ni pamoja na; Hisabati, Kingereza, Sayansi, Maarifa ya Jamii, Historia, Maarifa ya Jamii, Jiografia, Tehama, Uraia, Uraia na Maadili, Stadi za Kazi, Haiba na Michezo, Kiswahili, Afya na Mazingira na Sayansi na Teknolojia.

Aghalabu, katika shule zote 30 hakuna hata shule moja yenye vitabu vya masomo yote vya darasa la 2, 3 na 4, hii ni kutokana na maboresho ya Sera ya Elimu yaliyofanyika mwaka 2014 na kuanzishwa kwa mtaala mpya ulioanza utekelezaji wake mapema mwaka 2015. Mtaala huu ulilenga kupunguza idadi ya miaka ya mwanafunzi kukamilisha mzunguko wake wa kielimu kwa ngazi ya msingi kutoka miaka saba (yaani darasa la 1-7) na kufikia miaka sita (yaani darasa la 1-6).

Uanzishwaji na utekelezwaji wa mtaala huu ulikuwa na changamoto zake, kubwa zaidi ikiwa ni hii ya kutokuwepo vitabu vya kutosha vinavyoshabihiana na maono ama dira ya mtaala husika hivyo walimu hulazimika kutumia uzoefu tu kufundisha ilihali mitihani hutungwa kwa kufuata mtaala husika.

Kwa upande wa shule za sekondari za umma, Kati ya shule zote 20, ni shule 16 tu zenye vitabu vya masomo yote, yaani, Fizikia, Bailojia, Kingereza, Hesabu, Jiografia, Kemia, Uraia, Kiswahili, Historia, Biashara, Uhasibu pamoja na Fasihi.

Aidha, Miongoni mwa shule hizo, hakuna hata shule moja yenye vitabu vya kutosha vya masomo ya sayansi, yaani, Fizikia, Kemia, Hesabu, Bailojia na Jiografia. Hivyo basi, utafiti huu tuliofanya utakuwa ndio mwanga katika kuongoza taasisi nyingine nyingi kufanya tafiti nyingi juu ya mahusiano ya hali hii na adhima tuliyojiwekea katika kuifikia nchi ya uchumi wa kati, nchi ya viwanda. Tunapaswa kujiuliza:

- Je, tunawezaje kuifikia adhma hii ilhali hali ni ya namna hii?
- Hivyo viwanda vitaongozwa na wataalamu gani iwapo sisi hatutajiandaa vya kutosha katika kuwapata wataalamu hao?
- Mwisho tujiulize, Je, ni nini hasa matokeo ya hali hii? (Swali hili tunalijibu katika kipengele kinachofuata hapa chini).

## *2.0: NINI MATOKEO YA HALI HII KATIKA AFYA YA ELIMU NCHINI?*

Kama tulivyoona hapo kabla, maktaba zina mchango na nafasi kubwa sana katika ustawi wa elimu na maendeleo ya nchi. Afya ya elimu yetu kwa kiasi kikubwa inategemea uwepo wa vitabu vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia, sambamba na hapo hutegemea zaidi uwepo wa maeneo maalumu yenye utulivu wa hali ya juu ambayo kimsingi, mwanafunzi mmoja mmoja ama kikundi watakutana kujadili masuala yote yahusuyo masomo kwa usaidizi kutoka katika vitabu vya aina tofauti tofauti. Eneo hili ndilo haswa wanazuoni huliita maktaba.

Kutokana na takwimu tulizozionyesha hapo juu, Afya ya Elimu yetu kwa sasa si shwari, hii inatokana na uwepo wa shule nyingi kutokuwa na maktaba na vitabu vya kutosha. Itakumbukwa kuwa, ni kwa kupitia vitabu tunaweza kupata maarifa tofauti tofauti hasa yanayogusa maisha yetu ya kila siku, changamoto tunazozipitia na namna ya kukabiliana nazo kufikia maendeleo tuliyoyakusudia. Katika maisha ya 'Uanafunzi', vitabu humsaidia mwanafunzi kuweza kupata maarifa yatakayomsaidia na kumwezesha kufanya vizuri katika mitihani yake ya ndani na ile ya kitaifa. Hivyo basi kutokuwepo kwa maktaba na vitabu vya kutosha mashuleni kunahatarisha upatikanaji wa elimu bora miongoni mwa wanafunzi na hii inaweza kuwa na athari zifuatazo kwa wanafunzi na hata jamii;

i. Kutasababisha kupotea kabisa kwa utamaduni wa kujisomea kwa lengo la kutafuta maarifa.
ii. Wanafunzi wengi wataendelea kufanya vibaya katika mitihani yao ya kitaifa. Hii pia itasababisha taifa kuendelea kuwa na wimbi la wajinga na watu wasiojua kusoma wala kuandika, tofauti na miaka ya nyuma. Kwa mujibu wa sensa ya Taifa ya Mwaka 2012, Takwimu zinaonyesha kuwa kiwango cha watu wazima wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu ni asilimia 85% mwaka 1995 na 77.9% mwaka 2013. BEST 2016 wanaeleza kuwa kiwango cha ufaulu wa kidato cha nne mwaka 2008 kilikuwa ni asilimia 83.6% huku mwaka 2016 kikishuka na kufikia asilimia 70%.
iii. Kushuka kwa kiwango cha uelewa wa mambo mbalimbali miongoni mwa wanafunzi na wanajamii. Hapa ndipo naukumbuka msemo wanaopenda kuutumia wataalamu kuwa: Maarifa mengi yapo kwenye vitabu hivyo

ukitaka kufanikiwa zaidi kifikra huna budi kuwa mpenzi wa usomaji wa vitabu.

iv. Kutokana na athari namba (iii) hapo juu, hali hii pia itasababisha uzalishaji wa vijana na jamii ya watu wasiojitambua katika kusimamia mambo mbalimbali yanayowagusa katika maisha yao ya kila siku,

v. Kuna hatari kubwa ya taifa kuwa na kizazi ambacho asilimia kubwa huishia njiani bila kukamilisha mzunguko wao wa kielimu kutokana na kutoweza kufaulu mitihani yao kutokana na sababu ambazo kimsingi tuna uwezo wa kuzitatua. Madhara ya jambo hili ni taifa kutopata wataalamu wa kutosha katika kutunga na kusimamia sera zilizopo, mathalani, Sera ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2014/15-2024/25 iliyoazimia kuiweka nchi katika uchumi wa kati wa viwanda.

Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2014,Takwimu za elimu zinaonyesha kuwa idadi ya watoto wanaojiunga na elimu ya awali ni asilimia 24.7% mwaka 2004 na 37.3% mwaka 2013. Kiwango cha watoto walioandikishwa elimu ya msingi ni 77.6% kwa mwaka 1995 na 96.2 mwaka 2013, huku kwa mwaka 2000 hadi 2012 wastani wa asilimia 5% tu ya wahitimu wa darasa la 7 ndio waliofanikiwa kuendelea na masomo kwa ngazi ya Sekondari (O-Level) na Sekondari ya juu (A-Level). Wakati huo huo, kati ya hizo asilimia 5% ni asilimia nne (4%) tu ya wanafunzi hao ndio hufanikiwa kuendelea hadi ngazi ya Chuo Kikuu. Katika wimbi kubwa lililobaki hutupwa nje ya mfumo katika mtihani wa taifa wa darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita na wengine huacha shule kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo magonjwa, vifo na kushindwa kumudu gharama za elimu.

## *3.0: MCHANGO/NAFASI YA MAKTABA KATIKA KUKUZA MAENDELEO YA ELIMU NA NCHI KWA UJUMLA*

Kutokana na takwimu ambazo tumekwisha zionesha hapo juu, na hali halisi tuliyoiona juu ya kutokuwepo kwa maktaba mashuleni na athari zake, ni vema tukatambua na kuelewa kwamba: tutakuwa sio waungwana na wenye mapenzi

mema na nchi yetu kama tusipoona haja ya kuwa na maktaba za umma ambazo zitasaidia kwa kiwango kikubwa wanafunzi wetu kufanya vizuri katika mitihani yao ya ndani na kitaifa na zitakazokuwa pia msaada kwa jamii nzima ambapo yote haya yataleta mchango chanya kwa taifa letu. Kwa ujumla wake, maktaba hizi zitakuwa chachu katika kuyafikia yafuatayo;

i. Uwepo wa maktaba utawapa fursa wanafunzi kupata sehemu ambayo watakutana vikundi ama mtu mmoja mmoja kwa lengo la kujisomea. Faida ya hili ni kuwa wengi wa wanafunzi wataweza kufanya vizuri katika mitihani yao ya ndani ya shule na ile ya kitaifa na pia kupanua uelewa na uwezo wao wa kudadavua mambo yanayoigusa jamii yao.
ii. Kuongeza utendaji wa wanafunzi katika nyanja/ngazi zote za kielimu (yaani, msingi, sekondari na hata chuo.
iii. Itarejesha na kuimarisha tabia ya kujenga mazoea ya kujisomea miongoni mwa wanafunzi na wanajamii.
iv. Itaongeza ari na tabia ya wanafunzi kujitafutia maarifa nje ya mtaala wa darasani.
v. Itasaidia kutatua changamoto zinazozikumba shule zetu nchini kama vile uhaba wa vitabu vyote kwa shule za msingi na hasa vya sayansi kwa sekondari kama nilivyokwisha viainisha hapo juu.

Jambo la muhimu ni kuwa, faida zote hizi zitatuelekeza katika kufikia taifa makini lenye wananchi makini ambao tumejidhatiti kuyafikia malengo tuliyojiwekea. Zaidi, ni vema tukaelewa kuwa maktaba haiishii tu kumsaidia mwanafunzi kuweza kupata maarifa yatakayomwezesha kufanya vizuri katika masomo yake, bali maktaba pia huenenda sambamba na kumtengeneza mwanafunzi na jamii kuweza kujitambua kupitia maarifa mbalimbali ambayo watu huyapata katika usomaji wa vitabu na hivyo kuwawezesha wanajamii kuweza kufikiri, kutenda na kung’amua mambo kwa namna pana. Na hivyo, kumfanya mwanafunzi kuwa mahiri katika nyanja mbalimbali za kimaisha mara baada ya kuhitimu masomo yake.

*4.0: JE, NDOTO YA KUWA NA MAKTABA ZA UMMA KWA KILA KATA INAWEZEKANA?*

Katika swali hili, jibu la haraka ni NDIO INAWEZEKANA. Rasimali za vivutio tulivyonavyo pekee pasina kuangalia njia nyingine za uzalishaji mali tulizo nazo zinatosha kabisa kulithibisha jibu hili.

Ndugu msomaji wa makala haya, hapa nimekuwekea rasilimali hizo, tafadhali zipitie kisha nawe utoe jibu lako kama inawezekana au haiwezekani kuwa na maktaba za umma za kisasa katika kila kata nchini.

Kwa mujibu wa *Taarifa ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara 1961-2011* rasilimali hizo ni kama ifuatavyo:

- Tuna Mbuga kubwa za Savana zenye mito, mabonde, milima na maziwa.
- Tuna mlima Kilimanjaro, ambao pamoja na kuwa mlima mrefu kuliko yote Afrika (wenye mita 5,895) pia ni mlima mrefu kuliko yote duniani ambayo inasimama pekee bila ya kuambatana na safu za milima mingine kama ilivyo mlima Everest.
- Kuna maziwa makuu matatu yenye sifa za pekee duniani:
    i. Ziwa Victoria lililoko upande wa Kaskazini ni kubwa kuliko yote Afrika na la tatu duniani miongoni kwa maziwa yenye maji baridi.
    ii. Ziwa Tanganyika lililoko upande wa Magharibi ni la kwanza kwa urefu Afrika na la pili kwa kuwa na kina kirefu duniani.
    iii. Ziwa Nyasa lililoko upande wa Kusini Magharibi ni mojawapo ya maziwa yanayotajwa duniani kwa kuwa na kina kirefu.

Pamoja na maziwa hayo makuu matatu yanayotupa umaarufu na sifa nyingi Afrika na duniani yapo maziwa mengine maarufu ndani ya nchi yetu yanayopatikana ndani ya mipaka ya nchi yetu ambayo ni pamoja na Rukwa, Eyasi na Manyara.

Nchi yetu ndio chanzo cha mito mikubwa mitatu maarufu barani Afrika ambayo ni Nile, Kongo na Zambezi. Baadhi ya mito inayomwaga maji yake katika mito hii

maarufu imeanzia katika miinuko iliyoko Kaskazini Magharibi na Kusini Magharibi mwa nchi yetu.

Tuna bonde la Ngorongoro lililopo upande wa Kaskazini Mashariki ambalo limeingia kwenye maajabu saba ya dunia kutokana na maumbile yake na hazina ya wanyamapori waishio katika hifadhi hiyo.

Tuna hifadhi ya Serengeti iliyo jirani na Bonde la Ngorongoro ni maarufu duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wanyama wakubwa, hususan, tembo, faru, twiga, simba na mbogo.

Kutokana na uhamaji wa mamilioni ya nyumbu kutoka hifadhi yetu ya Serengeti kwenda mbuga ya Masai Mara nchini Kenya na kurudi kumetutambulisha duniani na kuwa mojawapo ya maajabu mapya nane ya dunia.

Hifadhi zote kwa pamoja nchini zina zaidi ya asilimia 20% ya wanyama wote wakubwa barani Afrika. Nne kati ya hifadhi hizo, yaani Ngorongoro, Serengeti, Selous na Mlima Kilimanjaro zinatambulika rasmi duniani kuwa ni kati ya urithi muhimu wa binadamu. Mapokeo mengine yenye hadhi hii hapa nchini ni pamoja na bonde la Oltupai zamani 'Olduvai Gorge' (ambalo lipo ndani ya hifadhi ya Serengeti na ambalo ndiko kulikogunduliwa masalia ya binadamu wa kale yenye umri mkubwa kuliko yote yanayojulikana duniani hadi hivi sasa), masalia ya miji ya Kale ya Kilwa na Songo Mnara, na michoro ipatikanayo kwenye miamba iliyoko maeneo ya Kondoa.

Tuna Hifadhi ya Kitulo ambayo husifika kwa kuwa na vivutio vya ndege na maua ya aina ya kipekee duniani. Pia tuna tumekuwa na hifadhi nyingi za misitu ambazo kwa ujumla wake zinachukua asilimia 38.9 ya eneo lote la nchi.

Pia Tanzania tunajulikana duniani kutokana na kugunduliwa kwa masalia ya mnyama wa kale mkubwa aitwae Dinosoria (Dinosaur). Makadirio ya wanasayansi yanathibitisha kuwa Dinosoria huyo aliyetoweka duniani na ambaye masalia yake yaligunduliwa mwaka 1909 katika eneo la Tendaguru, mkoani

Lindi, alikuwa na urefu wa mita 23, kimo cha mita 13 na uzito usiopungua kilogram 30,000.

Tuna eneo la bonde la mto Kihansi lililopo Wilayani Kilombero, Morogoro, ni sehemu pekee duniani yenye vyura wadogo waitwao Kihansi Spray Toads. Vyura hawa ni wa kipekee kwa sababu huzaa watoto moja kwa moja badala ya kutaga kwanza mayai kama wafanyavyo vyura wengine.

Tumejaliwa pia kuwa na rasilimali nyingi za asili, zikiwemo ardhi yenye rutuba, aina nyingi za madini, maji na viumbe mbalimbali vya nchi kavu na baharini.

Pamoja na vivutio vyote hivyo nilivyoviainisha, bado Tanzania tunaongoza kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii barani Afrika.

Ukiachilia mbali hivi vivutio vya kitaifa, zipo pia rasilimali mbalimbali ambazo zinazizunguka jamii zetu tunamoishi. Ingetosha kabisa kushikamana kwa pamoja kuhakikisha kwamba kupitia rasilimali hizo tunazitumia katika kuanzisha ama kuendeleza miundombinu mbalimbali kama vile maktaba, zahanati n.k katika jamii zetu.

Sasa swali ni kwamba kwa nini kama Watanzania bado tumeshindwa kutoa huduma muhimu na za msingi kama elimu kwa ubora wake?

Jibu hapa ni jepesi tu:

- HATUNA WASIMAMIZI AMBAO WANA WELEDI katika kuzisimamia rasilimali zetu ili kuwezesha kunufaika nazo.
- Sera ya uchangiaji wa gharama za elimu iliyoanza kutekelezeka miaka ya 1990 ndio mwanzo wa haya yote kwani ndio ilipanda mbegu ya ubidhaishaji wa elimu nchini uliojenga matabaka katika upatikanaji wa elimu bora. Shule binafsi zilipata elimu bora kutokana na kuinunua huduma hii kwa gharama kubwa huku shule za umma zikizidi kushika mkia kutokana na waliopewa dhamana ya kuzisimamia rasilimali za umma kushindwa kuzisimamia rasilimali hizo vizuri kwa maslahi ya umma.

- Viongozi, wadau wa elimu na mashirika ya kitaifa na kimataifa yasiyo na nia njema na sisi yalizidi kuipalilia na kuimwagilia maji mbegu hii na hatimaye sasa imemea na kuwa mti mkubwa ambao sasa tayari umewaangukia na kuwalalia wanyonge ambao hawana uwezo wa kupeleka watoto wao hizo shule za binafsi zenye vifaa vya kutosha vya kujifunzia na kufundishia na zenye mazingira rafiki yanayowawezesha wanafunzi katika safari yao ya kitaaluma.
- Sambamba na hayo, sisi kama jamii (mimi na wewe) kwa namna moja ama nyingine tumesinzia ama kupuuzia katika kuhakikisha jamii yetu inakuwa na huduma mbalimbali za msingi, mathalani, hili la kuwa na maktaba.
- Kiufupi ni kwamba tumebweteka na kuwa tegemezi kwa viongozi wa serikali tukisubiri kila kitu wafanye wao hali ambao itatulazimu kusubiri miaka mingi sana kwa jamii zetu kuweza kuwa na miundombinu mizuri inayokidhi haja.

## *5.0: NINI KIFANYIKE?*

Ili kuwezesha uanzishaji, uboreshaji na uendelezaji wa maktaba zilizo bora nchini kwa angalau kila kata, wadau tuliowafikia kwa mjumuisho wao, wamependekeza haya yafuatayo;

i. Uwepo usimamizi madhubuti wa rasilimali zetu ili kuminya njia za ufujaji wa mapato. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa fedha za kutosha ambazo zitasaidia katika kuanzisha, kuboresha na kuendeleza maktaba za umma nchini.
ii. Serikali, wadau, asasi za kiraia na mashirika ya ndani na nje ya nchi kwa pamoja tushirikiane katika kuanzisha, kuboresha na kuendeleza maktaba za umma nchini.
iii. Jamii nzima ya Watanzania bila kujali makundi yetu, tushirikiane katika kupinga ubidhaishaji wa elimu nchini. Kwa kukataa Sera hii kutasaidia watoto wa Tabaka zote kupata elimu iliyo sawa na yenye ubora.

iv. Kila mwananchi kwa nafasi yake tujipime na kujitathmini kuangalia ni kwanamna gani sote tunaweza kuwa chachu ya uanzishwa, uboreshwaji na uendelezwaji wa huduma mbalimbali muhimu za kijamii kama vile maktaba za umma. Tuangalie namna ya kujiunga na kisha kuhakikisha tunaweka mikakati madhubuti ya upatikanaji wa huduma hizi bila utegemezi kutoka kwa viongozi wa kisiasa. Hili litajenga heshima kwetu na uthamini wa huduma hizo tulizoziweka kwa nguvu zetu. Ni imani ya kila mmoja kwamba sisi tukianza na kusimama wenyewe, viongozi watajifunza na kuwa weledi katika kuleta maendeleo kwa kuhakikisha tunakuwa na miundombinu ya kutosha na iliyo bora.

Ni rai yetu kwamba, ikiwa tumedhamiria kufikia nchi ya uchumi wa viwanda hatuna budi kujidhatiti kuwekeza katika elimu kwanza. Tuwekeze nguvu zetu katika kuhakikisha tunaboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kujenga vyumba vya madarasa vya kutosha, maji na umeme, tunaboresha mazingira ya ujifunzaji na kuhakikisha pia tunakuwa na vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na uwepo wa maktaba za kutosha zenye vitabu vya kutosha ili kuwawezesha wanafunzi wetu kujifunza na kupata maarifa ya kutosha kulingana na ngazi walizopo kielimu. Sambamba na hilo pia, itawajengea wanafunzi na jamii nzima mazoea ya kupenda kujisomea kwa lengo la kujitafutia maarifa na kuongeza ufahamu juu ya mambo mbalimbali.

Sambamba na hapo tukisema tunataka kufikia kuwa nchi ya viwanda lazima tuhakikishe tunakimbizana na sayansi na teknolojia kwa kuandaa madarasa maalumu ya kujifunza TEHAMA (Teknolojia, Habari, Mawasiliano). Madarasa haya yawe na vifaa vya kutosha kama vile kompyuta n.k.

Mwisho, ikiambatana na hayo yote hapo juu, lazima tuhakikishe kuwa tuna walimu wa kutosha wenye ujuzi ambao watatusaidia kama taifa kuzalisha wataalamu wa kutosha kuweza kutatua changamoto zinazotukabili kufikia nchi ya viwanda na kama jamii tujiwekee utaratibu wa kujisomea. Wanasaikolojia wanaamini kwamba; "Ili ubongo uweze kufanya kazi vizuri, uwe na manufaa kwa

binadamu, ni sharti uendelezwe, unolewe pamoja na kulindwa". Haya yote yatawezekana ikiwa ubongo huu unasaidiwa na chachu ya usomaji wa vitabu, kutizama na kusikiliza mambo ya msingi ambapo haya yote yanatuelekeza kupiga hatua kimaendeleo ya kisiasa, uchumi na kiutamaduni.

**MAARIFA NI NGUVU, TUPAMBANE KUJIFUNZA.**

----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Mwandishi wa Makala hii anapatikana kwa mawasiliano yafuatayo:
Barua pepe: gibson@tsnp.or.tz; **Simu : +255 676 108 116/ +255 766 548 471.**